Mkombozi
Empower. Engage. Enable.

Muhtasari wa Utafiti



Sensa 2006:

Yanayosemwa na ukweli ulivyo kuhusu watoto wa mitaani wa Tanzania

Ujenzi wa kijamii wa "tatizo" unaficha ukweli wa mahitaji ya haraka ya sera na huduma kwa ajili ya watoto walio katika mazingira magumu

Utangulizi:

Mkombozi ni asasi ya kipekee Tanzania ambayo kila baada ya muda (2003, 2005 na 2006) hufanya sensa ya watoto na vijana ambao wanaonekana mitaani katika miji ya Moshi na Arusha. Majumuisho haya yanatoa maelezo mafupi ya mambo yaliyojitokeza ya sensa ya 2006, ambayo yalipima mielekeo na hali ya watoto wa mitaani na kutoa mwanga kuhusu mitindo yao ya kimaisha na mikakati wanayotumia watoto na vijana wanaotumia muda wao mitaani. Katika jitihada za kuwagawa watoto na kuwatofautisha kati ya wale wanaoishi mitaani na wale wanaokuja mitaani kwa muda tu, waliohojiwa waliulizwa: "Wewe unaishi na kulala mitaani wakati wote, mchana na usiku?" Jibu lilipokuwa hasi waliulizwa: "unakuja mitaani wakati wa mchana na kurudi nyumbani usiku?" Wahojiwa waliulizwa walikuwa wakijishughulisha na nini kila siku, na kupima muda wanaotumia kwa kutumia kipimo cha likert. Mkombozi ilikuwa na haja ya kutumia fursa ya sensa hii kuzidisha uelewa wake kuhusu unyanyasaji wa watoto, na kuchunguza uhusiano unaoweza kuwapo kati ya manyanyaso ya watoto majumbani na kukimbia kwao kwenda mitaani (mwenendo huu umeelezwa katika harakati zetu ndani ya miaka 10 iliyopita). Tukichukua baadhi ya maswali kutoka utafiti wa Adverse Childhood Experience (ACE), tuliwauliza watoto maswali ambayo yalionyesha nia ya kumlinda mtoto kuliko manyanyaso yaliyo wazi. Pia tuliwapa watoto fursa ya kutojibu swali hili kama hawapendi.

Maelezo ya kitarakimu:

Matokeo ya sensa yanawakilisha mwenendo chanya miongoni mwa watoto wa mitaani katika miji yote miwili kati ya Januari 2006 na Oktoba 2006:

- Isipokuwa kwa nyongeza ya 26% ya watoto na vijana wanaoku ja mitaani kwa muda wa mchana tu mjini Moshi (kutoka 301 hadi 411) vikundi vingine vyote vimepungua: kumekuwa na upungufu wa 70% miongoni mwa watoto na vijana wanaoishi mitaani mchana na usiku mjini Arusha (kutoka 522 hadi 467); kumekuwa na upungufu wa 11% wa watoto na vijana wanaoku ja mitaani kwa muda mchana mjini Arusha (kutoka 522 hadi 467); kumekuwa na upungufu wa 51% ya watoto na vijana wanaoishi mitaani wakati wote mjini Arusha (kutoka 354 hadi 173 mwaka 2006).
- 10% ni wasichana na 90% ni wavulana.
- Mwenendo wa watoto na vijana wanaokuja mitaani mchana kufanya kazi, kwa ajili ya burudani au kuomba unaendelea kuwazidi watoto na vijana wanaoishi muda wote katika mazin gira ya mitaani.
- Mjini Arusha 96% ya watoto wanaoishi mitaani muda wote wana umri zaidi ya miaka 15, kutoka 62% mwaka 2005.
- Mjini Moshi 54% ya watoto wanaoishi mitaani muda wote wana umri zaidi ya miaka 15.

P.O. Box 9601 Moshi, Tanzania ■ Tel: (255) 27 2754793 ■ Fax: (255) 27 2753410 ■ info@mkombozi.org ■ www.mkombozi.org

Sifa za watoto na vijana wa mitaani:

Sensa hii inatupa picha kwa ufupi ya maisha na matarajio ya watoto na vijana wa mitaani Kaskazini mwa Tanzania. Picha inayoonekana inapingana na mitizamo iliyopo inayowabagua watoto na vijana hawa kama wasiosikia, wahalifu na wasiokubalika katika jamii. Kusema kweli mjini Moshi na Arusha:

- 36% ya watoto na vijana walisema kuwa wanatumia muda wao kufanya kazi, 77% wamesema wanafanya hivyo kwa zaidi ya muda wa saa 12 kwa siku.
- 24% wamesema kuwa wanatumia muda wao wakiomba, 75% wanafanya hivyo kwa zaidi ya muda wa saa 12 kwa siku.
- 5% tu ya wale wanaolala mitaani mjini Arusha walikiri kuwa wanatumia dawa za kulevya, na hakuna aliyekiri hivyo mjini Moshi.
- Mjini Moshi hakuna kijana aliyekiri kuhusika na umalaya, ambapo Arusha vijana wanane walikiri kuhusika, na waliutafsiri umalaya kama kazi (wasichana 5 na wavulana 3).
- 13% ya watoto wanaoishi mitaani wakati wote walidai kuwa wanahudhuria shule za msingi kila siku, kama walivyodai 17% ya watoto wanaokuja mitaani kwa muda wa mchana tu. Hii sio kawaida, tukichukulia tunavyofikiri kuwa maisha ya mitaani hayatoi nafasi ya kuhudhuria shuleni, na inasababisha utafiti zaidi ili kuelewa jinsi watoto hawa wanavyoweza kuendesha maisha yao na elimu.
- 30% ya watoto na vijana walikuwa wamemaliza elimu ya msingi karibuni.

Watoto wanaponyanyaswa majumbani mwao na katika jamii zao hakuna nyenzo, taratibu au hatua zinazoweza kusaidia kuzuia manyanyaso hayo au kuwasaidia watoto kurekebika kutokana nayo. Sensa hii imegundua kuwa:

- Wastani wa 53% ya watoto na vijana wote wa mitaani walisema kuwa wazazi wao au mtu mzima mwingine nyumbani wali watukana, waliwagombeza, waliwadharau au waliwafanyia mambo ambayo yangeweza kuwaumiza kimwili.
- 28% ya watoto na vijana wote waliohojiwa walisema kuwa hakukuwa na chakula cha kutosha majumbani mwao hata kidogo.
- 26% walisema kuwa ulevi wa wazazi wao uliingilia matunzo yao mara kwa mara.
- 44% ya waliohojiwa waliathirika na ugomvi au walishuhudia ugomvi wakati fulani.
- 14% walisema kuwa mara nyingi walikuwa wameogopa sana, wenye msongo wa muda mrefu, wanatishika sana au wanahofia usala ma wao.

Vitongoji vya Moshi na Arusha ni vyanzo vizuri vya watoto na vijana wa mitaani. Mjini Arusha asilimia zifuatazo za watoto na vijana wa mitaani (wa wakati wote au wa muda wa mchana tu) zimetoka katika vitongoji vifuatavyo: Arusha Ngaramtoni = 12% (125); Arusha Ngarenaro = 9% (91); Arusha Unga Ltd = 8% (83); Arusha Esso = 7% (68); Arusha Majengo = 8% (78).

Vilevile vitongoji vya Moshi pia ni vyanzo vya watoto wa mitaani. Vitongoji hivyo ni: Moshi Njoro = 18% (187); Moshi Pasua = 10% (100); Moshi Kiboriloni = 7% (70); mitaa 6 inayounda kata ya Majengo inaendelea kuwa chanzo cha pamoja cha watoto wa mitaani kikiwa na jumla ya 13% (131).

Hii yote inamaanisha nini?

Hatuamini kuwa hii ina maana halisi ya kupungua kwa watoto na vijana walio katika mazingira magumu. Bali tunaamini kuwa badiliko hili linaonyesha kukua kiumri kwa watoto.

Kuna mambo yanayoonekana kujitokeza. Kwanza, kadri umri wa watoto na vijana unavyoongezeka, tunaona vijana balehe na wanaoanza kuwa watu wazima wanaongezeka wakitegemea mazingira ya mitaani kwa maisha yao. Wametumia sehemu kubwa ya maisha yao ya utotoni na ya balehe katika mazingira haya, na wakati wakiimarisha mbinu zao za kuishi, wamekosa elimu na fursa za maendeleo ambazo zingewawezesha kufanya vizuri zaidi katika mkondo mkubwa wa jamii. Hii ina matokeo katika aina ya msaada wanaohitaji ili waweze kuhama kutoka mitaani na kuweza kufanya vizuri zaidi katika jamii. Sensa hii inaimarisha yaliyojitokeza katika utafiti uliofanywa Kenya (Ayuku at al, 2003) ambao unasema ni muhimu kuweka bayana tofauti iliyopo miongoni mwa watoto wa mitaani na kwa mipango na sera zinazotaka kufuatwa kwa ajili ya vikundi mbali mbali. Msaada wa mbinu za biashara, upatikanaji wa mikopo, msaada wa wana rika, na uhusiano na watu wazima ambao ni mfano mwema, vyote ni mikakati ambayo itawezesha vijana hawa kuingia upya katika mkondo wa jamii.

Uzoefu wa Mkombozi ni kuwa pale palipo na umoja katika jamii, watoto wanakuwa wakijaliwa sana na kulindwa kutokana na manyanyaso. Sensa ya 2006 inabaini kuwa vitongoji vya Moshi na Arusha kwasasa ni vyanzo muhimu vya watoto na vijana wanaokuja mitaani. Wazazi wengi wasio na wenzi wao na familia ndogo zisizo na ukoo wanaishi katika maeneo haya na huduma za kijamii hazitoshi na ni duni. Ingawa kuna msururu wa sababu zinazomfanya mtoto aamue kuondoka au kutoondoka nyumbani na kwenda mitaani, Mkombozi inaona kuna mchanganyiko wa hali ya kiuchumi na kuondokana na mazingira ya familia za manyanyaso kama mambo ya msingi yanayowafanya watoto na vijana waingie mitaani.

Watoto na vijana wanaendelea kukimbilia mijini kutafuta ajira na fursa. Kusema kweli wengi wa vijana hawa wanachukua mwelekeo wa kutumia fursa katika mazingira yao wakiiona mitaa ya mijini kama njia ya kuwafikisha wanakotaka waende na kupata maendeleo.

Kuhitimisha:

Mkombozi inaamini kuwa kuna hazina kubwa na ambayo kwa kiwango kikubwa haijaguswa waliyonayo vijana hawa, na kwamba kuwasaidia kuipata ni sehemu kubwa ya mchakato wa kuwarekebisha (Kidd & Kraal, 2003).

Wakati tunafahamu matatizo yaliyopo katika kuondoka mitaani mara tu kijana anapozama ndani ya utamaduni huo, sisi na asasi nyingine tunahitaji kufanya utafiti, utetezi kwa ajili ya sera na maendeleo ya huduma zinazowasaidia watoto na vijana walio katika hatari ya kukosa makazi.

Mkombozi inatetea kuwa tunahitaji kulishughulikia suala la watoto na vijana walio katika mazingira magumu si kama tatizo ambalo watu wanaadhibiwa na kutengwa, bali linatokana na kushindwa kwetu katika kuwa na sera na kukosa kuwekeza katika huduma ya: elimu, ulinzi wa watoto, fursa za ajira na burudani kwa vijana.